NDOA NA TARATIBU ZAKE

SHERIA KATIKA LUGHA RAHISI

KIMETOLEWA NA CHAMA CHA WANASHERIA TANZANIA BARA KWA UFADHILI WA TAASISI YA LEGAL SERVICE FACILITY (LSF)

DISEMBA, 2015

NDOA NA TARATIBU ZAKE

SHERIA KATIKA LUGHA RAHISI

KIMETOLEWA NA CHAMA CHA WANASHERIA TANZANIA BARA KWA UFADHILI WA TAASISI YA LEGAL SERVICE FACILITY (LSF)

DISEMBA, 2015

KIMEANDALIWA NA
Chama Cha Wanasheria Tanzania Bara
Kiwanja Na. 391, Mtaa wa Chato
Regent Estate, S.L.P 2148
Dar es Salaam, Tanzania.
Simu +255 22 2775313 / +255 22 5500002
Nukushi +255 22 2775314
Barua Pepe info@tls.or.tz
Tovuti www.tls.or.tz

© Chama Cha Wanasheria Tanzania Bara, 2015

Waandishi
- Kaleb Gamaya,
- Mackphason Buberwa
- Stephen Msechu
- Celina Kibasa
- John Mwang'ombola
- Alphonce Gura
- Judith Kapinga

Wahariri
- Magdalena A. Mlolere,
- Stephen Msechu

Kimeandikwa na kuhaririwa chini ya usimamizi wa;

Kamati ya Msaada wa Sheria
- Anna Kulaya-Mwenyekiti
- Butamo Philip
- Daniel Lema
- Donesta Byarugaba
- Fulgence Massawe
- Maria Matui

Kamati ya Utafiti na Machapisho
- Prof. Cyriacus Binamungu
- Dr. Alex Makuklilo
- Dr. Lilian Mongela
- Dr. Ally Possi
- Madeline Kimei
- Daniel Welwel

Yaliyomo

Shukrani iv
Utangulizi 1
Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 1
Aina za Ndoa 1
Sifa za Kufunga Ndoa..... 2
Haki na Wajibu wa Wanandoa 4
Haki za Mwanamke katika ndoa 7
Mamlaka za Ufungishaji Ndoa 8
Usajili wa Ndoa..... 9
Faida za Kusajili Ndoa..... 10
Talaka 11
Taratibu za kuomba talaka..... 11
Ndoa za Utotoni/Ndoa Katika Umri Mdogo..... 13
Baadhi ya Sababu ya Ndoa za Utotoni..... 14
Madhara ya Ndoa katika Umri Mdogo..... 16
Tufanye nini kukabiliana na ndoa za umri mdogo?..... 19

Shukrani

Kamati ya Msaada wa Sheria ya Chama Cha Wanasheria Tanzania Bara inatoa shukrani za pekee kwa wadau mbalimbali kutoka mashirika ya kutoa msaada wa kisheria kwa ushauri wao maridhawa katika kuandaa kijarida hiki cha ***Ndoa na taratibu zake***.

Pili, Shukrani ziende kwa Taasisi ya Legal Service Facility (LSF) kwa ufadhili na ushauri wa kipekee katika kuandaa kijarida hiki.

Pia Kamati inatoa shukrani za dhati kwa Baraza la Uongozi la Chama cha Wanasheria chini ya Rais Charles Rwechungura na Sekretariat ya Chama chini ya Kaleb Gamaya kwa rasilimali na ushirikiano waliotoa katika kukamilisha kazi hii muhimu kwa taifa letu inayolenga kukuza uelewa wa sheria miongoni mwa wananchi.

Utangulizi

Sheria ya ndoa ya mwaka 1971, Sura ya 29 inatoa mwongozo kuhusu haki na wajibu kwa wanandoa, utaratibu kuhusu jukumu la malezi, haki na maslahi ya watoto wa ndoa. n.k. Sheria hii inatambua ndoa za kimila, ndoa za kidini na ndoa za kiserikali zinazofungwa bomani. Sheria imetambua tofauti hizi kwa kuzingatia maslahi na utofauti wa kiutaratibu wa maisha ya wanajamii.

Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971

Sheria hii ndiyo inayoshughulikia mahusiano ya wanandoa (mke na mume) nchini Tanzania.

Maana ya Ndoa

Kwa mujibu wa sheria hii, ndoa ni muungano wa hiari kati ya mwanamke na mwanaume unaokusudiwa kudumu kwa muda wa maisha yao yote.

Utambuzi wa ndoa (Aina za ndoa na sifa za kufunga ndoa)

Kisheria ndoa hutambulika pale ambapo watu wawili kwa hiari yao wataamua kuungana chini ya mamlaka husika. Watu wanaoishi bila ndoa hawatakuwa na haki kama zile za wanandoa, mfano juu ya mali walizochuma. Mtu yoyote kati yao ana uwezo wa kupinga kwa kutoa sababu kwamba hawakuwa kwenye ndoa.

Aina za Ndoa

Kuna aina kuu mbili za ndoa:-

(i) Ndoa ya mke mmoja; na
(ii) Ndoa ya wake wengi.

Taratibu za kufunga ndoa hizi zaweza kuwa:-

(i) Kimila;
(ii) Kidini [kikristo au kiislamu] na/au
(iii) Kiserikali.



Sifa za Kufunga Ndoa

Ili ndoa iweze kuwa halali kisheria, wanaokusudia kufunga ndoa ni lazima wazingatie mambo yafuatayo;

Ndoa lazima iwe ya Hiari Muungano wa ndoa kati ya mwanaume na mwanamke ni lazima uwe wa hiari kwa pande zote mbili. Hivyo basi, hiari iliyopatikana kwa njia ya udanganyifu, ulaghai, kwa kurubuni au kulazimisha, haiwezi kisheria kuhesabika kuwa hiari kwa kuwa haikutolewa kwa uhuru. Na hivyo muungano kati ya watu hao wawili hautahesabika kuwa ni wa hiari na unaweza kuifanya ndoa kuwa batili. Mmoja wa wanandoa anaweza kwenda kwenye mamlaka husika na kuomba ndoa ibatilishwe.

Muungano lazima uwe kati ya mwanamke na mwanaume: Sheria za Tanzania inatambua ndoa kama muunganiko wa hiari baina ya mwanamke na mwanaume. Muunganiko wowote tofauti na huo unavunja sheria za nchi

Umri: Umri unaokubalika kisheria ni miaka 18, ila binti anaweza kuolewa akiwa chini ya umri huo lakini si chini ya umri wa miaka 15 kwa idhini ya wazazi/walezi wake; Ikiwa umri wake ni chini ya miaka 14 basi kibali maalumu kitatolewa na mahakama. Wanaharakati wa Haki za binadamu wamekuwa wakikosoa kifungu hiki kwa kuwa kinaleta ubaguzi na kuruhusu binti kuolewa akiwa mtoto hivyo kumvunjia haki zake za mtoto na haki za binadamu

Muungano wa ndoa uwe wenye kutazamiwa kudumu: Sheria ya Ndoa inasema muungano wa mume na mke uwe unakusudiwa kuwa wa kudumu mpaka pale kifo kitakapowatenganisha au endapo, kwa dini ya Kiislamu, kutatolewa talaka. Ndoa za muda mfupi kama vile za mikataba kwa mujibu wa sheria ya ndoa ya Tanzania hazikubaliki.

Wanandoa wasiwe maharimu (ndugu wa damu): Kwa mujibu wa sheria hii, hairuhusiwi baba na binti, mama na mwana, babu na mjukuu, au bibi na mjukuu, kaka na dada, kuoana

Wanandoa ni lazima wawepo wakati ndoa ikifungwa. Wanandoa wote ni lazima wawepo wakati wa tukio la kufunga ndoa. Hata hivyo, sheria inaruhusu ndoa kufungwa katika mazingira ya mwanandoa mwingine kutokuwepo ikiwa kuna sababu za msingi. Hata hivyo, ni lazima mwanandoa huyo awe ametoa idhini hiyo mbele ya mashaidi.

Kuwepo na Mashahidi: Hawa lazima wawe watu wenye akili timamu na wawe na umri wa miaka 18 na kuendelea. Mashahidi wanatakiwa wasiwe chini ya watu wawili

Kusiwe na ndoa inayoendelea: Kwa wakristo hairuhusiwi kufunga ndoa zaidi ya mke mmoja, na kwa waislamu wanaruhusiwa kuoa si zaidi ya wake wanne.

Mfungishaji ndoa lazima awe na mamlaka: Mfungishaji ndoa ni lazima awe na leseni au kibali cha kufungisha ndoa kutoka kwa msajili wa ndoa. Hata hivyo, ndoa iliyofungwa na mtu asiye na leseni kisheria si batili ikiwa haitapingwa na mtu yeyote mahakamani.

Mwanamke asiwe katika Eda: kwa mujibu wa sheria za kiislamu, mwanamke wa kiislamu hatakiwi kufunga ndoa awapo kwenye eda ya kufiwa na mume au wakati ameachana na mume wake.Eda ni kipindi cha miezi 3kinachotolewa kwa mwanamke wa kiislamu aliyeachika katika ndoa au aliyefiwa na mumewe, ili taratibu fulani za kidini zifanyike.Kama mwanamke ambaye ndoa ilifungwa Kiislamu anaolewa wakati wa kipindi cha Eda hakijaisha basi ndoa hiyo ni batili. Lakini mfaruku au mtalikiwa awe anafuata dini ya Kiislamu. Kama atabadili dini baada ya kufiwa au kupewa talaka masharti ya Eda hayatambana.

Ndoa itangazwe kwa muda wa siku 21 na kusiwe na pingamizi: Wanaotazamia kufunga ndoa wasiwe wamewekewa pingamizi la msingi na mtu yeyote. Sheria ya ndoa inatamka wazi kwamba kabla ya ndoa kufungwa lazima tangazo litolewe kuonyesha kusudio la kufunga ndoa. Tangazo lazima liwe la siku 21 kabla ndoa husika kufungwa, lakini pia sheria inamruhusu msajili wa ndoa kufungisha ndoa bila tangazo la siku 21 kama kuna sababu za msingi.

Haki na Wajibu wa Wanandoa

Sheria ya ndoa imeainisha haki na wajibu mbalimbali kwa wanandoa kama ifuatavyo:-

(i) **Matunzo:** Mume anawajibu wa kumtunza mkewe kwa malazi, mavazi na chakula kulingana na kipato chake. Wajibu huu huhamia kwa mke pindi mume wake anaposhindwa kuutimiza kwa sababu

za msingi kama vile kuugua.Hata hivyo, ni muhimu kukumbuka kuwa, mke ambae anauwezo wa kuingiza kipato, anao wajibu wa kuchangia katika kutunza familia na si kumuachia mume peke yake.

(ii) **Kuishi katika nyumba ya ndoa**: Nyumba ya ndoa ni ile wanayoishi wanandoa na inaweza kuwa nyumba waliyojenga au kupanga. Ikiwa nyumba hiyo imejengwa na wanandoa hakuna mwenye mamlaka ya kuiuza au kuiweka rehani kwa ajili ya kuchukua mkopo benki bila idhini ya mwanandoa mwenzake.

(iii) **Kumiliki mali:** Sheria hii inatoa haki sawa kwa mume na mke kumiliki mali aidha kwa pamoja au kila mmoja na mali yake. Inapotokea ndoa kuvunjwa mahakamani mgawanyo wa mali utategemea na mchango wa kila mwanandoa katika upatikanji wa mali hiyo. Ikiwa mwanandoa atasema hakuchuma mali hiyo kipindi cha ndoa basi atapaswa athibitishe hilo. Ikiwa itathibitika kuwa alipata mali hiyo kabla ya ndoa au kipindi ambapo wanandoa walikuwa wametengana basi mali hiyo inaweza kuwa ni yake binafsi. Hata hivyo ifahamike kuwa mwanandoa mmoja kutokuwa na kipato haiwezi kufanya kuwa asipate mgao, kwakuwa alihusika katika njia nyingine ya kutoa mchango kama vile kutunza watoto, kuiweka nyumba katika hali ya usafi, kuitunza n.k

(iv) **Dhana ya mkopo:** Mke ana haki ya kukopa kwa jina la mume wake au kuuza vitu vya mume kwa lengo la kuipatia familia mahitaji muhimu ikiwa mume hatoi mahitaji hayo bila sababu za msingi.

(v) **Matunzo ya watoto wa ndani ya ndoa:** Ni wajibu wa mwanaume kutunza watoto wake bila kujali anaishi nao au la. Hii ni pamoja na gharama za chakula, mavazi na shule.

(vi) **Uhuru wa kuishi popote**: Endapo mume atafariki basi mwanamke anao uhuru wa kuishi popote na anayo haki ya kuolewa au kutokuolewa.

(vii) **Kufanya tendo la ndoa:**Wanandoa wanao wajibu wa kutimiza tendo la ndoa ikiwa hakuna udhuru wa ugonjwa au sababu zingine.

(viii) **Wajibu wa kuzaa:** Ikiwa mwanandoa (ambaye ni mke) anao uwezo wa kubeba mimba au kutunga mimba (akiwa mwanaume), ni wajibu wake kuzaa. Kuzuia kwa makusudi kutozaa ndani ya ndoa husababisha migogoro ya ndoa na kufanya ndoa kuvunjika. Hivyo wanandoa wanapaswa kujadiliana na kukubaliana wakati wa kuzaa, idadi ya watoto wanaotaka kuzaa na muda wa kusubiri kabla ya kupata mtoto mwingine.

Ndoa batili: Ndoa batili ni ndoa ambayo si halali kisheria toka kufungwa kwake. Vitu vinavyofanya ndoa kuwa batili kama vifuatavyo;

- Mmoja au wanandoa hao hawakufikisha umri unaotambulika kisheria wa kufunga ndoa
- Kama wanandoa hao ni maharimu
- Kama mmoja wa wanandoa hao alikuwa na ndoa inayoendelea (alishaoa au kuolewa)
- Mmoja au wanandoa hao walilazimishwa kuoa au kuolewa
- Mmoja au wanandoa hao hakushiriki katika sherehe ya kufungwa ndoa hiyo
- Kama mfungishaji wa ndoa hiyo hakuwa na mamlaka kisheria ya kufungisha ndoa hiyo
- Kama ndoa hiyo ilifungwa kwa malengo kwamba itakuwa ni ya muda mfupi (ya mkataba)

Ndoa Batilifu: Ndoa batilifu ni ndoa ambayo itachukuliwa kisheria kuwa ni ndoa halali hadi hapo amri ya kuivunja itakapotolewa na mahakama. Ndoa batilifu ni halali kama ndoa nyingine isipokuwa ina kasoro fulani. Wanandoa katika ndoa hii wana haki na wajibu sawa kama ilivyo katika ndoa nyingine zisizo na kasoro.

Kadhalika watoto waliozaliwa katika ndoa ya namna hii ni halali na wana haki zote kisheria.Vitu vinavyofanya ndoa kuwa batilifu ni kama vifuatavyo;

- Mwanandoa kutoweza kufanya tendo la ndoa.
- Mmoja wa wanandoa kudhihirika kuwa na kichaa au kifafa.
- Mmoja wa wanandoa kuthibitika kuwa na magonjwa ya zinaa.
- Mke kudhihirika kuwa alikuwa na mimba ya mwanaume mwingine wakati wa kufunga ndoa.
- Mwanandoa mmoja wapo kukataa kwa makusudi kufanya tendo la ndoa tangu ndoa kufungwa.

Angalizo: Hata hivyo, ndoa batilifu itaendelea kuwa ndoa halali kisheria mpaka pale mmojawapo atakapoamua kupeleka malalamiko mahakamani na mahakama kuibatilisha baada ya kupata uthibitisho wa sababu yoyote kati ya hizo tajwa hapo juu.

Haki za Mwanamke katika ndoa

Mwanamke alie katika ndoa ana haki sawa kama zile za mwanaume ikiwa ni pamoja na haki ya;

- Kununua, kumiliki au kuuza mali zake mwenyewe
- Kukopa kwa jina la mume wake kwa ajili ya kuihudumia familia yake
- Kudai au kupokea mshahara wa mume wake kwa ajili ya kuitunza familia yake pale ambap mume wake hawezi kutimiza wajibu huo

- Kuuza mali ya familia kwa ajili ya kuihudumia familia
- Kutonyanyaswa au kupewa adhabu za kutandikwa viboko
- Kupendwa, kutunzwa na kuhifadhiwa kulingana na uwezo wa mume

Angalizo: mwanamke pia ana wajibu wa kumtunza na kumhifadhi mume wake pale ambapo mume wake ni mgonjwa au ameshindwa kufanya shughuli zake kwa sababu ya kuumia au kutokuwa na kazi inayomuingizia kipato.

Mamlaka za Ufungishaji Ndoa

Sheria imebainisha na kutoa nguvu kwa mamlaka zifuatazo kuwa na uwezo wa kufungisha ndoa. Watu ambao wanahitaji kufunga ndoa wanaweza kwenda kwenye mamlaka zifuatazo:

(i) Msajili mkuu au Msajili msaidizi katika ofisi za Wilaya/ Manispaa

(ii) Viongozi wa dini katika Makanisa na Msikiti
(iii) Viongozi wa mila katika kabila/kijiji

Mahari
Mahari siyo kigezo cha kufungisha ndoa. Jambo la msingi ni kwamba wanaokusudia kufunga ndoa wawe wametimiza sifa za kufunga ndoa mfano umri, hiari n.k

Dhana ya Ndoa
Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 inatambua kuwepo kwa dhana ya ndoa kwa mujibu wa kifungu cha 160. Kwa mujibu wa kifungu hiki, sheria ya ndoa inaeleza kwamba watu wawili (mke na mume) ni wanandoa ingawa hawajafuata taratibu zozote za kufunga ndoa iwe kimila, kidini au kiserikali.

Na ili mke/Mume aweze kuithibitishia mahakama kuwa alikuwa anaishi kwenye dhana ya ndoa, mambo yafuatayo ni muhimu.
(i) Kwamba wanandoa walipoanza kuishi kwenye dhana ya ndoa, hawakuwa na ndoa inayoendelea;
(ii) Wanandoa hao wanaishi/waliishi kwa pamoja kwa muda wa miaka miwili mfululizo na jamii inayowazunguka inawatambua kuwa mume na mke;
(iii) Wanandoa hao wametimiza umri unaokubalika kisheria ambao ni miaka 18.

Angalizo: Dhana ya ndoa inaweza kukanushika mahakamani ikiwa mmoja wa wenzi hao atatoa ushahidi wa kuonyesha kuwa hawakuishi kama mke na mume au muda wa miaka miwili haukutimia.

Dhana hii ya ndoa husimama pale tu ambapo hakuna mmoja kati ya wenzi hao wawili aliyekuwa na ndoa inayoendelea wakati akiingia katika mahusiano hayo. Kwa hiyo, kimada au 'nyumba ndogo' ya mtu mwenye ndoa hawezi kudai haki ya 'dhana ya ndoa'.

Usajili wa Ndoa

Sheria ya ndoa inamtaka kila mwanandoa kusajili ndoa yake katika mamlaka husika ndani ya siku 30 baada tu ya kufunga ndoa. Ndoa za aina zote zinatakiwa kusajiliwa kwenye mamlaka husika na kutolewa cheti cha ndoa.

- Kama ndoa ilifungwa kimila, au kiislamu, na kama msajili hakuwepo, mwanandoa atatakiwa kwenda kusajili ndoa hiyo kwa Msajili wa wilaya au kwa kadhi (kama ni ndoa ya kiislamu) ndani ya siku 30.

Ndoa ambazo zimefungwa muda mrefu pia zinaweza kusajiliwa kama haikusajiliwa kabla.

Faida za Kusajili Ndoa

- Usajili wa ndoa na cheti cha ndoa unarahisisha taratibu na mashauri yanayohusu mirathi kwa kujua aina ya ndoa na yupi ni mke/mme halali, hivyo kusaidia kulinda haki ya mjane na mgane.
- Pia katika mashauri ya talaka, cheti kitahitajika mahakamani katika kuthibitisha mzazi halali wa mtoto na kuamua juu ya nani atakaa na mtoto.
- Cheti cha ndoa kinahitajika katika sehemu nyingi zinazochangia kujenga uchumi wa familia, kama vile wakati wa kuuza ardhi, kuomba mikopo benki n.k
- Pia usajili wa ndoa na cheti cha ndoa unawatambulisha wanandoa kimataifa pale watakapohitaji kusafiri kwenda nchi za nje.
- Pia inasaidia katika kuweka ushahidi kwamba watu hawa ni wanandoa, na kusaidia katika regista na kumbukumbu za taifa.
- Umiliki wa mali – kusajili ndoa yako kunasaidia katika kutambulisha wanandoa halali, hii itasaidia katika kujua nani ana haki ya kumiliki mali za ndoa. Wanandoa wana haki sawa ya kumiliki mali walizonazo ndani ya ndoa.

Talaka

Maana ya Talaka

Kwa mujibu wa dini ya kiislamu ndoa inaweza kuvunjwa kwa njia ya talaka. Hata hivyo kwa mujibu wa Sheria ya Ndoa, ndoa itahesabika kuwa imevunjika ikiwa imevunjwa na mahakama pekee

Kwa maana hiyo, talaka inaweza pia kutafsiriwa kuwa ni ruhusa ya kisheria ambayo mahakama hutoa kwa mume au mke kumwacha wanandoa mwenzake

Sababu za Kutoa Talaka

Mahakama hutoa talaka inapoona na kuridhika kuwa ndoa imevunjika kiasi ambacho haiwezi kurekebishika tena. Ili kuthibitisha kuwa ndoa imevunjika na haiwezi kurekebishika tena, mahakama hutumia vigezo vikuu vifuatavyo:-

i. Ukatili: unaweza ukawa wa maneno kama vile matusi au ukawa wa matendo (kama vile kwa mwanandoa);
ii. Uasi/utoro;
iii. Ugoni/kufumaniwa;
iv. Kulawiti/kuingilia kinyume na maumbile;
v. Kutotimiza tendo la ndoa kwa makusudi;
vi. Kutengana kwa zaidi ya miaka mitatu (3);
vii. Kifungo cha mwenza kisichopungua miaka mitano (5) au cha maisha;
viii. Dhana ya vifo kwa kipindi kisichopungua miaka mitano (5);
ix. Kichaa kisichotibika na kiwe kimethibitishwa na madaktari bingwa wa magonjwa ya akili wasiopungua wawili.

Taratibu za kuomba talaka

Kwa utaratibu wa kisheria, mwanandoa anayetaka kupata amri ya mahakama ya kuvunja ndoa yake anapaswa afanye yafuatayo;-

i. Atapeleka malalamiko yake kwenye Baraza la Usuluhishi la Ndoa linalotambulika kisheria. Mabaraza hayo ni BAKWATA,

baraza la ndoa la kanisa, baraza la kata na baraza la kamishna la ustawi wa jamii.

ii. Baraza likishindwa kusuluhisha wanandoa litatoa hati ya kwenda mahakamani.

iii. Akipata hati hiyo ya kushindikana kwa usuluhishi atafungua shauri la kutaka talaka mahakamani, ataomba mali walizochuma zigawanywe na pia ataomba mahakama ielekeze jinsi uangalizi na malezi ya watoto yatakavyokuwa.

iv. Ataambatanisha orodha ya watoto wa ndoa na umri wao katika hati ya kudai talaka.

v. Ataambatanisha pia orodha ya mali za wanandoa hao walizochuma pamoja wakati wa ndoa yao.

Angalizo: ndoa yoyote haiwezi kuvunjwa hadi iwe imefikisha muda wa miaka miwili, labda kuwe na sababu nzito ambayo inaweza kuishawishi mahakama kutoa hati ya talaka kabla ya ndoa kutimiza miaka miwili.

Uangalizi na Matunzo ya Watoto Baada ya Ndoa Kuvunjika

Kwa kawaida mzazi yoyote anaweza kuomba apewe amri ya kukaa na mtoto baada ya ndoa kuvunjika. Mahakama ndio yenye mamlaka ya kuamua mtoto ataishi na nani pindi ndoa inapovunjwa na baada ya ndoa kuvunjika. Amri ya kubeba dhamana ya malezi ya mtoto/watoto inaweza kutolewa kwa baba, mama au ndugu wa karibu wa mtoto/watoto.

Haitajalisha mtoto/watoto watakaa na nani, mume na mke watatakiwa kuchangia kutoa matunzo kwa ajili ya watoto, na kuhakikisha haki zao za msingi kama elimu, chakula, mavazi, kutibiwa, hazipotei.

Ndoa za Utotoni/Ndoa Katika Umri Mdogo

Ndoa za utotoni ni nini?
Mtoto ni mtu yeyote mwenye umri chini ya miaka 18. Hivyo basi ndoa za utotoni ni kitendo cha kuishi maisha ya mke na mume na mtu mwenye umri chini ya miaka 18. Ufungishaji wa ndoa kwa watu walio chini ya umri wa miaka 18 ni ukiukaji wa haki za mtoto.

Tanzania ni miongoni mwa nchi zinazoongoza kwa ndoa za utotoni duniani. Tafiti mbalimbali zinaonesha kuwa mnamo mwaka 2010, asilimia 37 ya wanawake wenye umri wa miaka 20 hadi 24 waliotolewa kabla ya kufikisha miaka 18. Maana yake ni kwamba wasichana wawili (2) kati ya watano (5) nchini Tanzania waliolewa wakiwa watoto.

Kwa mujibu wa Chama cha Wanahabari Wanawake Tanzania (TAMWA) ndoa za umri mdogo zinaonekana ni jambo la kawaida nchini Tanzania. Mikoa inayoongoza kwa ndoa za utotoni ni Shinyanga (asilimia 59), Tabora (asilimia 58), Mara (asilimia 55), Dodoma (asilimia 51), Lindi (asilimia 48), Mbeya (asilimia 45), Morogoro (asilimia 42), Rukwa (asilimia 40), Ruvuma (asilimia 39), Mwanza (asilimia 37), Kagera (asilimia 36), Mtwara (asilimia 35), Manyara (asilimia 34), Pwani (asilimia 33), Tanga (asilimia 29), Arusha (asilimia 27), Kilimanjaro (asilimia 27), Kigoma (asilimia 26), Dar es Salaam (asilimia 19), na Iringa (asilimia 8).

Kikwazo kikubwa katika kupambana na tatizo la ndoa za utotoni ni sheria ya ndoa ya mwaka 1971. Sheria hii inaruhusu wasichana wenye miaka 14 kuolewa (kwa ruhusa maalum ya wazazi), inaruhusu wasichana wenye umri kuanzia miaka 15 kuolewa iwapo umbile lao linaonekana kubwa.

Baadhi ya Sababu ya Ndoa za Utotoni

Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971

Sheria ya ndoa hubagua kati ya wasichana na wavulana, ikitambua umri wa miaka 15 kama umri wa kisheria wa mwanamke kuweza kuolewa na umri wa miaka 18 kwa mwanaume kuweza kuoa. Sheria hiyo inaashiria kukubalika kwa dhana kwamba miaka michache baada ya kupevuka, wasichana huwa tayari kufanya ngono na kupata watoto, haya pia ndiyo mapokeo katika tamaduni nyingi hapa nchini

Mgongano/Mkinzano wa Sheria Hapa Nchini

Mgongano wa sheria hapa nchini kwa kiwango kikubwa pia unachangia kushamiri kwa ndoa za utotoni. Sheria ya mtoto ya mwaka 2009 haitaji moja kwa moja umri wa kuolewa, hata hivyo inafafanua kuwa mtoto ni mtu yeyote wa umri wa chini ya miaka 18. Kwa hali hiyo basi, sheria ya ndoa ya mwaka 1971 inaridhia moja kwa moja ndoa za utotoni.

Pia sheria ya kanuni za adhabu inawabagua wasichana kwa kuruhusu ndoa za umri mdogo mradi tu mke na mume hawatafanya tendo la ndoa hadi wafikishe umri wa miaka kumi na tano au zaidi na wawe hawajatengana. Kumpa majukumu ya ndoa mtoto wa kike kabla ya kufikisha umri wa miaka 18 ni kumbagua na kumnyima fursa sawa za elimu, ukuaji na afya ya akili, afya ya uzazi, na kufurahia utoto wake sawa na mwenzie wa jinsi ya kiume.

Kumaliza mgogoro wa ukatili wa kijinsia

Familia za wahalifu wa ukatili wa kijinsia pamoja na waathirika (watoto wa kike chini ya miaka 18) huamua kumaliza mgogoro kwa kuoana, ikiwa na maana kwamba mwathirika huolewa na mbakaji.

Ulinzi

Wakati mwingine wazazi huamini kwamba ndoa hizi zinawalinda wasichana hasa pale wanapoona kwa kufanya hivyo huenda wanawaepusha wasichana na ukatili wa kimwili au kingono. Hata hivyo dhana hii si ya kweli hata kidogo kwani tafiti zinaonesha kuwa wasichana walioolewa kwenye umri mdogo wamekuwa wakipata mateso makubwa kwenye ndoa zao ikiwemo kupata mimba za utotoni ambazo wakati mwingine husababisha vifo na maradhi ya kudumu

Umasikini
Kwa baadhi ya familia masikini sana mahari inayolipwa, kama chanzo cha mapato kwenye familia na wazazi huamini kuwa kwa kumuozesha binti katika umri mdogo kunapunguza mzigo na gharama kwa familia kwani baba anakuwa amepunguza idadi ya watu wa kuwalisha, kusomesha na kutunza

Mila na desturi
Ndoa za utotoni kwenye Mila na desturi za makabila mengi ya Tanzania zinatokea kwa sababu tu ni utamaduni. Kwa sababu eti imekuwa hivyo katika jamii zetu vizazi kwa vizazi basi tuendeleze ndoa za utotoni. Ikumbukwe kuwa tamaduni, mila na desturi zililetwa na watu/binadamu na zinaweza kubadilika. Huko nyuma mababu na mabibi hawakufahamu madhara ya ndoa za utotoni na mazingira ya ulimwengu yamebadilika sana. Kizazi hiki cha sasa kina wajibu wa kuachana na utamaduni huu unaombagua mtoto wa kike.

Majukumu ya Kijinsia
Kwenye jamii nyingi nchini ambako ndoa za utotoni zimeshamiri watoto wa kike wanabaguliwa na kutothaminiwa sawa na wenzao wa jinsi ya kiume. Mara nyingi huonekana kama mzigo kwa familia kutunza na kusomesha. Jitihada zifanyike kubadili mitazamo na kusisitiza kuwa watoto wa kike ambao hawaozwi wakiwa na umri mdogo na wamemaliza masomo yao bila kukatishwa kwa sababu yeyote ile wana nafasi kubwa ya kutoa mchango kwenye maendeleo ya familia na jamii.

Madhara ya Ndoa katika Umri Mdogo

Vifo kutokana na mimba za utotoni
Wasichana wanaoolewa katika umri mdogo wako katika hatari kubwa ya kupoteza maisha kutokana na kupata mimba katika umri mdogo. Tafiti zinaonesha kuwa wajawazito wengi wanaopoteza maisha wakati wa kujifungua ni wale walio na umri chini ya miaka 18. Aidha, watoto

wachanga wanaozaliwa na mama mwenye umri mdogo wanakabiliwa na hatari kubwa zaidi ya kupoteza maisha kuliko wale waliozaliwa na mama wa umri mkubwa. Wataalamu wanasema miongoni mwa kila vichanga 1,000 vinavyozaliwa na mama wa umri wa chini ya miaka 18, vichanga 41 hupoteza maisha ndani ya mwezi mmoja baada ya kuzaliwa. Hata hivyo mama anapokuwa na umri wa miaka 20 hadi 29, idadi ya vifo vya vichanga hupungua hadi kufikia vifo 22 kwa kila vichanga 1,000 vilivyozaliwa hai. Pia kutokana na kupata mimba wakiwa watoto mno katika ndoa zao mara nyingi wasichana hukatiza masomo yao na kukosa haki ya kupata elimu, uhuru wa kiuchumi, na hukabiliwa na unyanyasaji wa majumbani kwa sababu ya hali yao ya ujauzito ikiwemo ubakaji wa kwenye ndoa.

Ongezeko la hatari za kiafya

Hatari kadhaa za kiafya pia huwakabili wasichana wanaoolewa katika umri mdogo ikiwemo kupasuka mirija ya uzazi, mimba kutunga nje ya mfuko wa uzazi, kupata fistula (Kwa kitaalamu fistula hujulikana kama njia isiyo ya kawaida inayounganisha mfuko wa mkojo na uke, ambayo huruhusu mkojo na/au haja kubwa kutoka kwenye kuta za uke bila mwanamke kuwa na uwezo wa kujizuia. Fistula hutokea baada ya mwanamke kupata madhara wakati wa kujifungua pale ambapo kichwa cha mtoto ni kikubwa kuliko njia ya uzazi. Mimba katika umri mdogo hasa kutokana na ndoa za utotoni ni chanzo kikubwa cha tatizo la Fistula. Pia ndoa za utotoni zinaongeza athari ya maambukizo ya VVU na UKIMWI kwa wasichana kwani mara nyingi hawana sauti kwenye ndoa kuweza kufanya maamuzi ya kutumia kinga wakati wa tendo la ndoa.

Kumnyima mtoto wa kike haki ya kupata elimu

Haki ya Elimu ni haki ya kikatiba nchini Tanzania. Ibara ya sita (6) ya katiba inaeleza kuwa “Kila mtu nayo haki ya kujielimisha na kila raia atakuwa huru kutafuta elimu katika fani anayoipenda hadi kufikia upeo wowote kulingana na stahili na uwezo wake.” Hata hivyo watoto wa kike wamekuwa wakikatizwa masomo yao au kutopelekwa shuleni

kabisa (na wazazi au walezi wao) ili kuwaoza. Tafiti zinaonesha kuwa uwiano wa watoto wa kike na kiume hupungua kadri wanavyoendelea na masomo ingawa wakati wa uandikishaji uwiano huwa sawa. Kupungua kwa uwiano mara nyingi husababishwa na wasichana kukatizwa masomo kwa ajili ya kuolewa au kupata mimba. Huu ni uvunjaji wa haki za binadamu, kuvunja katiba ya nchi na kukiuka sheria za nchi zinazotoa haki sawa ya elimu kwa watoto wa kike na wa kiume bila kujali jinsi zao au hali zao za kiafya, kiuchumi, kitamaduni na kisiasa. Ikumbukwe kuwa wahenga walinena "Elimu ni Ufunguo wa Maisha". Katika mfumo wa maisha ya mwanadamu elimu imekuwa nyenzo muhimu ya kumpa mwanadamu maarifa, ujuzi na stadi za kukabiliana na changamoto zinazomkabili binadamu katika mazingira anayoishi. Mtoto wa kike pia anahitaji nyenzo hii imsaidie kukabiliana na changamoto za maisha.

Umasikini

Kwa kuwa mara nyingi hukatizwa masomo hivyo kushindwa kuhitimu elimu yao wasichana wanaoolewa katika umri mdogo, mara hivyo hukosa uwezo wa kuchangia katika pato la kaya. Matatizo ya kiuchumi huwasababishia wasichana walio kwenye ndoa katika umri mdogo usumbufu mkubwa kwenye ndoa zao kwa kuwa tegemezi kupita kiasi kwa waume zao jambo ambalo huwaweka katika hatari zaidi ya kufanyiwa vitendo vya unyonyaji na ukatili.

Ukatili wa kijinsia

Wasichana kwenye ndoa za umri mdogo wako katika hatari ya kufanyiwa vitendo vya ukatili wa kijinsia kuliko kundi lolote lile kwa kuwa kwa umri wao mara nyingi hawawezi kujitetea dhidi ya vitendo vya ukatili mfano kupigwa au kulazimishwa ngono, mara nyingi hawana ufahamu wa haki zao na ni tegemezi kiuchumi.

Ubaguzi dhidi ya wasichana

Ndoa katika umri mdogo zinaongeza ubaguzi dhidi ya wasichana kwani sheria inaruhusu ndoa kwa wasichana wenye umri wa miaka15 kuolewa kukiwa na idhini ya wazazi na miaka 14 kwa idhini ya mahakama. Hata hivyo hakuna mahala popote pale sheria inataja mtoto wa kiume kupata idhini ya wazazi au mahakama pale anapotaka kuoa. Huu ni ubaguzi dhidi ya watoto wa kike na ni kuwanyanga'anya uhuru wa kufurahi haki zao utotoni kama ilivyoanishwa kwenye sheria ya mtoto ya mwaka 2009, ni uvunjaji wa katiba ya nchi inayotoa haki sawa kwa wanawake na wanaume na ukiukaji mkubwa wa haki za binadamu na haki za wanawake

Tufanye nini kukabiliana na ndoa za umri mdogo?

Ndoa za utotoni ni tatizo kubwa na itagharimu muda na fedha nyingi kulimaliza. Lakini jamii inaweza kutumia baadhi ya mikakati ifuatayo kupunguza tatizo hili. Mikakati hiyo ni:

- Wasaidizi wa kisheria wawajengee uwezo viongozi na wazee wa mila ili waelewe madhara ya ndoa za utotoni katika familia na jamii wanayoishi
- Wasaidizi wa kisheria waishawishi jamii kujenga tabia ya kuwashirikisha viongozi muhimu katika jamii wakiwemo wale wa kimila ili kuwe na uelewa wa aina inayofanana miongoni mwao kuhusu haki za wasichana na wanawake na athari za ndoa za utotoni kwa familia na jamii wanayoishi
- Elimu kwa jamii ili kubadili mitizamo, mila na desturi zinazochangia kushamiri kwa ndoa za umri mdogo
- Kushirikisha viongozi wa dini na kuwaomba watumie majukwaa yao siku za ibada kukemea ndoa za umri mdogo na kutoa elimu ya madhara ya ndoa hizi kwa waatharika.
- Kuwajulisha wanawake na wasichana haki zao za kikatiba na kisheria na kuwawezesha wasichana na wanawake kutetea haki hizo kwa njia ambayo ni sahihi na inakubalika na jamii zao

- Kuwashirikisha wanaume na watoto wa kiume kwenye ulinzi na utetezi wa haki za watoto wa kike kwa namna ambayo inakubalika na jamii
- Kujenga mahusiano bora na mamlaka husika kwenye jamii mfano serikali za vijiji, mitaa, idara za ustawi wa jamii, maendeleo ya jamii, viongozi wa kimila, wakunga wa jadi, mangariba n.k ili kwa pamoja kushirikiana kupinga na kutokomeza ndoa za utotoni
- Kutoa taarifa polisi au kwenye mamlaka nyingine mfano serikali ya kijiji pale inapobainika kuna ushahidi wa kumuoza mtoto chini ya umri mdogo au kumkatiza masomo mtoto wa kike au wa kiume kwa sababu yeyote ile
- Wazazi na wanajamii kuhakikisha kwamba watoto wa kike wanapata haki yao ya elimu na wanahitimu masomo yao sawa na wenzao wa jinsi ya kike
- Jamii kuendelea kuzisisitiza serikali za mitaa ili kuishawishi serikali kufanya mabadiliko kwenye sheria ya ndoa ya mwaka 1971 ili umri wa kufunga ndoa uwe miaka 18.

Angalizo: Ni muhimu pia kuwekeza kwa wasichana na wanawake ili wapate fursa za elimu na uwezo wa kujitegemea kiuchumi.

Chama Cha Wanasheria Tanzania Bara
Kiwanja Na. 391, Mtaa wa Chato
Regent Estate, S.L.P 2148
Dar es Salaam, Tanzania.
Simu: +255 22 2775313 /+255 22 5500002
Nukushi: +255 22 2775314
Barua Pepe: info@tls.or.tz
Tovuti: www.tls.or.tz